# HOTUBA YA DKT. AGNES KIJAZI, MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA KWENYE UFUNGUZI WA WARSHA YA WANAHABARI KUHUSU UTABIRI WA MVUA ZA MSIMU WA VULI; OKTOBA HADI DISEMBA, 2017, 30 AGOSTI, 2017 DAR ES SALAAM, TANZANIA

**Wakurugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,**

**Wanahabari kutoka Vyombo mbalimbali vya habari na Washiriki wa Warsha hii,**

**Wataam kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,**

**Mabibi na mabwana.**

**Habari za Asubuhi.**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kujumuika katika warsha hii ya wanahabari. Napenda pia kuwashukuru kwa kukubali wito wetu na kushiriki katika warsha hii ya kujadili utabiri wa mvua za msimu zinazotarajiwa kwa mwezi Oktoba hadi Disemba, 2017.

**Ndugu Wanahabari,**

Mamlaka ya Hali ya Hewa inatoa kipaumbele kuvishirikisha vyombo vya habari katika mpango mkakati wake wa usambazaji wa taarifa za hali ya hewa kwasababu kuu mbili. Kwanza; vyombo vya habari vinaaminika na wananchi kwa asilimia kubwa hivyo wanahabari wakizitoa taarifa za hali ya hewa kwa usahihi zitaweza kutumika vyema kwa maendeleo ya Taifa letu.

Pili; Pamoja na njia nyingine zilizopo za kusambaza taarifa za hali ya hewa, vyombo vya habari ndio njia pekee ambayo kwa hiyo Mamlaka inawafikia wananchi wengi kwa haraka zaidi. Hivyo wanahabari wakielewa umuhimu wa taarifa za hali ya hewa na kutoa kipaumbele kusambaza taarifa hizo kupitia vyombo vyao, tahadhari zinazotolewa na Mamlaka zitasaidia kupunguza majanga na hivyo kuokoa maisha ya watu na mali zao.

kwa kifupi ni kwamba, vyombo vya habari vinamchango mkubwa sana wa kufikisha taarifa za hali ya hewa kwa jamii na hivyo kuiwezesha jamii kuchukua tahadhari na hatua stahiki katika kujikinga na athari zinazotokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Kama tunavyofahamu kwamba taarifa za hali ya hewa ni muhimu katika kuandaa

mipango ya maendeleo pamoja na utekelezaji wake katika sekta mbalimbali hapa nchi.

**Ndugu Wanahabari**

Jukumu kuu la Taasisi za hali ya hewa Duniani limejengwa katika kutoa taarifa za hali ya hewa zinazozingatia mahitaji ya mtumiaji. Hali hii inazilazimu taasisi za hali ya hewa Duniani kuhakikisha zinajenga mazingira mazuri ambayo yanasaidia kuwepo kwa majadiliano kwa ajili ya kutambua mahitaji ya watumiaji wa taarifa za hali ya hewa. Taasisi hizi zinatakiwa kuwa na mfumo unaounganisha watoa huduma na watumiaji. Mfumo huu unahusisha kuwepo kwa njia bora na za kutegemewa za mawasiliano na mrejesho wa taarifa baina ya watumiaji na watoa huduma. Hali hii husaidia katika kuhakikisha taarifa zinaboreshwa na kukidhi mahitaji ya watumiaji na

hivyo kujengea jamii uwezo wa kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa.

**Ndugu Wanahabari**

Katika msimu wa mvua za *Masika uliopita (*katika kipindi cha miezi ya Machi hadi Mei, 2017) maeneo mengi ya nchi yetu yalipata mvua za chini ya wastani kama ilivyokuwa imeanishwa katika utabiri huo, mvua hizi hazikuwa na mtawanyiko mzuri. Hali hii ilisababishwa na kuwepo kwa mifumo ya hali ya hewa iliyokuwepo kwa kipindi hicho iliyopelekea ukanda wa mvua kutoimarika katika maeneo mengi ya nchi.

Hata hivyo, kwa maeneo ya ukanda wa pwani husuan mkoa wa Tanga kulitokewa vipindi vya mvua kubwa katika mwezi wa Aprili, 2017 ambavyo vilisababisha mafuriko na maporomoko

ya ardhi katika maeneo ya Lushoto ambapo kwa upande wa Visiwa vya Unguja na Pemba ili sababisha mafuriko, vifo na uharibu wa mali na miundombinu. Idara ya maafa kwa upande wa Zanzibar waliweka katazo la watoto kwenda shuleni hali ambayo ilionesha matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa katika kupunguza athari ambazo zingejitokeza

Maeneo mengine ambayo yaliathriwa na mvua hizo ni pamoja na mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Iringa.

**Ndugu wanahabari;**

Taratibu za kutoa utabiri zinaanzia kwa kuangalia mifumo ya hali ya hewa katika maeneo makubwa ambapo kwa upande wetu tunashiriki mikutano ya SADC na Pembe ya Afrika. Mwaka huu tulibahatika kuwa wenyeji wa Mkutano uliohusisha wataalam na wadau kutoka pembe ya

Afrika. Mkutano huo ulifanyika Zanzibar na ulifunguliwa na Mhe. Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (MB). Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri alisisitiza suala la kuhakikisha taarifa za hali ya hewa zinasambazwa na kuwafikia walengwa. Hivyo warsha hii ni ya muhimu ikizingatiwa Media ni Sekta muhimu katika usambazaji wa taarifa za hali ya hewa. Ni matumaini yangu kwamba tutakuwa na mjadala utakaowezesha taarifa ya utabiri wa mvua za vuli, 2017 kusambazwa kwa kiwango kikubwa na hivyo kutekeleza agizo alilolitoa Mheshimiwa Waziri.

**Ndugu wanahabari,**

Pamoja na kujadili njia bora za kusambaza taarifa za hali ya hewa, mtapata fursa ya kusikia uzoefu wa wanahabari walioshiriki utabiri wa kanda

uliotolewa Zanzibar. Vile vile mtapata fursa ya kujadili maneno yanayotumika kwenye utabiri ambayo yanaonekana si rahisi kueleweka. Nafurahi kuwajulisha kwamba tayari Mamlaka imekwisha wasiliana na Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) na wamekubali tuwasilishe maneno hayo ili yajadiliwe na kupatiwa tafsiri rahisi itakayoeleweka kwa watumiaji. Hivyo warsha hii pia ni fursa ya kuwezesha upatikanaji wa maneno yote magumu ili tuyawasilishe BAKITA.

**Ndugu Wanahabari,**

Katika kumalizia hotuba yangu napenda nichukue fursa hii kuwashukuru sana vyombo vyote vya habari hapa nchini, mmekuwa mkishirikiana na TMA kusambaza taarifa za hali ya hewa kwa viwango vya kuridhisha sana. Mrejesho ambao

tunaupata toka kwa watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ni uthibitisho tosha wa kazi nzuri inayofanywa na vyombo vya habari. Kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Hali ya Hewa ninapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwenu. ***Asanteni Sana.***

Baada ya maneno hayo ni fursa yangu sasa kutamka kwamba warsha hii ya wanahabari kuhusu ***''UTABIRI WA MSIMU WA MVUA ZA OKTOBA HADI DISEMBA, 2017 ''*** imefunguliwa rasmi.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza**